

EGW

AGOSTI 2019 | NAMBA 23

# MAMBO MUHIMU

Chapisho la kila Robo la Ofisi ya Tawi ya Ellen G. White Estate - Adventist University of Africa

# MIALE YA NURU

*Miaka 170 ya Huduma ya Uchapishaji*

Mwanzo wa Uchapishaji 2 | Uchapishaji wa Kazi za Kibiashara 4 | Makala ya Watoto 7




*Kutoka katika mwanzo huu mdogo ilioneshwa kwangu kuwa itakuwa kama miale ya nuru iliyokwenda ikizunguka dunia.*

# MWANZO WA UCHAPISHAJI

Dondoo zimechukuliwa kutoka kitabu cha *Christian Experience and Teachings of Ellen G. White*, uk. 128 –130

**Ellen G. White**

Katika mkutano uliofanyika Dorchester, Massachusetts, Novemba, 1848, nilikuwa nimeoneshwa mwonekano wa kutangazwa kwa ujumbe wa kutiwa muhuri, na wajibu wa ndugu katika kuchapa nuru iliyokuwa inaangaza juu ya njia yetu.

Baada ya kutoka kwenye njozi, nilisema kwa mume wangu: "Nina ujumbe kwako. Huna budi kuanza kuchapa gazeti dogo na kulituma kwa watu. Hebu na liwe dogo katika hatua za kwanza; lakini kwa kadri watu wanavyolisoma, watakutumia njia za kusaidia kuchapa, na kazi hiyo itakuwa ya mafanikio tangu mwanzo. Kutoka katika mwanzo huu mdogo ilioneshwa kwangu kuwa itakuwa kama miale ya nuru iliyokwenda ikizunguka dunia."

Wakati tulipokuwa Connecticut, majira ya kiangazi, mwaka 1849, mume wangu aliguswa sana kuwa wakati umewadia wa yeye kuandika na kuchapa ukweli wa leo. Alitiwa moyo na kubarikiwa sana kwa kadri alivyokuwa akiamua kufanya jambo hili. Lakini tena akawa kwenye mashaka na mkwamo kwa kuwa alikuwa hana pesa. Kulikuwa na wale waliokuwa na uwezo wa kiuchumi lakini waliamua kuuzuia. Baadaye katika hali ya kukata tamaa na akaamua kutafuta kazi katika shamba la nyasi ili aanze kukata nyasi.

Mara tu alipoondoka nyumbani zigo lilisogezwa juu yangu nami nikazimia. Ombi likatolewa kwa ajili yangu nikabarikiwa, nami nikachukuliwa kwenye njozi. Niliona kuwa Bwana alikuwa amembariki mume wangu kufanya kazi mwaka mmoja uliopita; ya kwamba alikuwa amefanya matumizi mazuri ya fedha alizoingiza, na ya kwamba angeweza kupewa mara mia katika maisha haya, na kama angekuwa mwaminifu, zawadi nono katika ufalme wa Mungu; lakini kwamba Bwana kwa sasa asingempa nguvu za kufanya kazi shambani, kwa kuwa alikuwa amempangia kazi nyingine ya kufanya, na kwamba kama akiendelea kufanya kazi shambani, atalazwa na magonjwa; lakini kwamba ni sharti aandike, aandike, aandike na kutembea kwa imani. Mara moja akaanza kuandika, na

alipofikia kwenye aya ngumu, tuliweza kuungana katika kumwomba Mungu ili tuelewe tafsiri ya Neno lake.

### "UKWELI WA LEO"


Siku moja katika mwezi Juni, mume wangu alileta kutoka Middletown nakala elfu moja za toleo la kwanza la gazeti lake. Mara kadhaa wakati mipango ikiandaliwa, aliweza kutembea kwenda Middletown, kwenda na kurudi, umbali wa maili nane, lakini siku hii alikuwa ameazima farasi wa ndugu Belden na kigari cha kukokotwa kwa ajili ya kubebea magazeti na kurudi nayo nyumbani.


Mapande makubwa mazuri ya karatasi zilizochapwa yaliletwa ndani ya nyumba na kulazwa sakafuni, na kisha kundi dogo la watu wanaovutiwa walikusanyika ndani, na tukapiga magoti kuzunguka zile karatasi, na kwa mioyo iliyonyenyekezwa na machozi mengi tulimtafuta Bwana ili kuruhusu baraka zake zituame juu ya wajumbe wale wa ukweli waliochapwa.

Tulipokwisha kuzikunja zile karatasi, na mume wangu alipozifunga na kuandika anuani juu yao kwa wote aliodhani wangeweza kusoma, akaziweka ndani ya mfuko, na kuzibeba akielekea ofisi ya posta iliyopo Middletown kwa miguu.

Mnamo mwezi Julai na Septemba, aina nne za magazeti zilichapwa Middletown. Kila toleo lilikuwa na kurasa nane. [ukubwa wa ukurasa ulikuwa inchi sita kwa nane na nusu.] Daima kabla ya magazeti kutumwa, yalimwagwa chini mbele za Bwana, na maombi ya dhati yaliyoandamana na machozi, yalitolewa kwa Mungu, ili kusudi baraka zake ziandamane na wajumbe hawa wa kimya. Mara tu baada ya kuchapa toleo la kwanza, tulipokea barua zikituletea fedha za kusaidia kuchapa magazeti, na pia [kutujulisha] habari njema za roho nyingi zilizoukumbatia ukweli.

Tangu kuanza kwa kazi hii ya kuchapa, hatukukoma katika kazi yetu ya kuhubiri ukweli, bali tulisafiri kutoka mahali pamoja hadi pengine, tukitangaza mafundisho makuu ambayo yalileta nuru kuu na furaha kwetu, ikiwatia nguvu waumini, ikisahihisha makosa, na kuleta utengamano kanisani. Ili kuendeleza taasisi za uchapishaji, na wakati huo huo kuendeleza utendaji wetu wa kazi katika maeneo mbalimbali, gazeti likawa likihamishwa kutoka sehemu moja hadi nyingine.






Bwana anatamani kwamba nyumba zetu za uchapaji zimshuhudie yeye

# UCHAPAJI WA KAZI ZA KIBIASHARA

(Imechukuliwa kutoka *Shuhuda kwa Kanisa*, Gombo la 7, uk. 162 – 168)

**Ellen G. White**

Bwana alielekeza kwamba nyumba za uchapaji ni lazima zianzishwe kwa ajili ya kusambazwa kwa ukweli wa leo na ili kushughulika na aina mbalimbali za biashara ambazo kazi hii inahusiana nazo. Wakati huo huo zinapaswa kuwa na ukaribu na ulimwengu, ili ukweli uweze kuwa kama nuru iliyowekwa kwenye kiango kusudi watoe nuru kwa wote katika nyumba. Bwana anatamani kwamba nyumba zetu za uchapaji zimshuhudie Yeye.

## ZISIPEWE KIPAUMBELE

Kwa namna ye yote ile taasisi za uchapaji zisijiingize sana kwenye shughuli za kibiashara. Wakati shughuli hizi zinapopewa kipaumbele, wale waliounganishwa na nyumba za uchapaji hupoteza uoni wa kusudi ambalo kwalo, nyumba hizo za uchapaji zilianzishwa, na kazi yao huanza kuharibika.

Ipo hatari kwamba mameneja ambao hali zao za kiroho zimepotoka wataingia katika mikataba ya kuchapa mambo yenye kutiliwa mashaka kwa lengo tu la kujipatia kipato. Kama matokeo ya kuziingiza kazi hizi ndani, makusudi ya kuanzishwa kwa ofisi za uchapaji yatapotea, na taasisi [hizi] zitaonekana zipo sawa na shughuli zingine za kibiashara zilivyo. Kwa njia hii Mungu atashushiwa hadhi yake.

Katika baadhi ya nyumba zetu za uchapaji kazi ya kibiashara inalazimisha kuwepo kwa ongezeko la kudumu la mitambo ya thamani na vifaa vingine. Gharama itakayohitajika hivyo huwa ni mzigo mzito wa kodi kwa rasilimali za taasisi, na kutokana na kuwepo kwa kiwango hicho kikubwa cha kazi, patahitajika siyo tu ongezeko la vifaa, lakini kundi kubwa la wafanyakazi wanaoweza kutiishwa sawasawa.

Inadaiwa kwamba kazi ya kibiashara ina manufaa ya kifedha kwa ofisi. Lakini mmoja aliye na mamlaka [Mungu] amefanya makisio sahihi ya gharama ya kazi hii katika nyumba za uchapaji zinazoongoza [katika

uchapaji]. Aliwasilisha uwiano wa kweli, ukionesha kwamba hasara itazidi kipato. Alionesha kwamba kazi hii inasababisha wafanyakazi kupelekeshwa kwa kasi isiyokoma. Katika mazingira haya ya haraka, machafuko na hali ya kidunia, uchaji Mungu wa kweli na moyo wa ibada hufifia.

Si lazima kwamba shughuli za kibiashara ziondolewe kabisa kutoka nyumba za uchapaji, kwa kuwa hii itafunga mlango dhidi ya miale ya nuru ambayo ingepelekwa kwa ulimwengu. Na muunganiko na wadau walio nje hautakiwi uwe wenye madhara kwa wafanyakazi. Lakini kila itakapoonekana inaingiliana na hali ya kiroho ya taasisi, hebu kazi hiyo ya nje iwekwe kando. Anzisha na kuendeleza kazi ile inayowakilisha ukweli. Hebu hii ndiyo iwe ya kwanza, na kazi ya kibiashara iwe ya pili. Utume wetu ni kutoa kwa ulimwengu ujumbe wa onyo na rehema.

## MACHAPISHO YA KUDHALILISHA

Wakati nyumba zetu za uchapaji zinapofanya kiasi kikubwa cha kazi za kibiashara, kuna hatari kubwa kwamba maandishi yasiyokubalika yataingizwa ndani. Wakati mmoja wakati mambo haya yalipoletwa kwangu, kiongozi wangu alimuuliza mmojawapo wa wale wanaoshika wadhifa wenye jukumu kubwa katika taasisi ya uchapaji: "Unapokea kiasi gani kwa malipo ya kazi hii?" Kiasi kinacholipwa kiliwekwa mbele yake. Alisema: "Hiki ni kiasi kidogo sana. Ukifanya biashara kwa namna hii, utapata hasara. Lakini hata kama utapata kiasi kikubwa, aina hii ya vitabu itachapwa kwa hasara kubwa tu. Mvuto kwa wafanyakazi utakuwa wa kushusha moyo. Ujumbe wote ambao Mungu atawapelekea akiwasilisha utakatifu wa kazi, utazimishwa na tendo lako la kukubaliana nao kuchapa vitu hivi."

Ulimwengu umefurika vitabu ambavyo ingekuwa vyema kama vingechomwa kuliko kusambazwa. Vitabu kuhusu vita ya Wahindi na mada za namna kama hiyo, vinavyochapwa na kusambazwa kama mkakati wa kujipatia fedha [na nyumba zetu za uchapaji] ni bora visingesomwa kabisa. Kuna nguvu ya kishetani ya kupumbaza kwenye vitabu hivyo. Uhusiano unaodhuru moyo wa uhalifu na watekelezaji wa uhalifu huo una nguvu ya kuloga kwa vijana wengi, ukiwachochea kutamani kujilinganisha na yule mwenye matendo maovu zaidi. Kuna kazi nyingi ambazo zipo kihistoria zaidi na ambazo mvuto wake ni mdogo tu. Uovu uliokithiri, ujeuri, na mazoea ya kiuasherati, vinavyooneshwa kwenye vitabu hivi vimetumika kama chachu katika akili nyingi, zikiongoza katika kutenda matendo hayo hayo [yanayosimuliwa humo]. Vitabu vinavyoelezea mazoea ya kishetani yanayotendwa na wanadamu vinasaidia kutangaza kazi hizi za uovu. Ufafanuzi wa kutisha wa uhalifu na huzuni zake visingepaswa kuingizwa maishani, na hakuna mwenye kuuamini ukweli wa wakati huu ambaye angekuwa sehemu ya kudumisha kumbukumbu zake.

Hadithi za mapenzi na za kipuuzi, na masimulizi ya kusisimua hupatikana katika daraja lingine la vitabu ambavyo ni laana kwa kila msomaji. Mwandishi anaweza kuambatanisha somo nzuri katika uandishi wake na anaweza akaingiza mawazo ya kidini, lakini bado kwa sehemu kubwa Shetani hujivika mavazi ya malaika kwa ufanisi mkubwa ili kuwadanganya na kuwanasa. Akili huwa imeathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na yale inayojilisha. Wasomaji wa visa vya kipuuzi na vinavyosisimua wanakuwa hawapo tayari kwa majukumu yaliyo mbele yao. Wanaishi maisha yasiyo halisi na hawana tamanio la kuyachunguza Maandiko, na kujilisha chakula cha mbinguni. Akili imedhoofishwa na kupoteza nguvu yake ya kutafakari matatizo makubwa yahusuyo majukumu na mustakabali wa maisha.

Nimeelekezwa kwamba vijana wanakabiliwa na hatari kubwa kutokana na usomaji usio makini. Shetani daima anawaongoza wote vijana kwa watu wazima kuvutiwa na hadithi zisizo na thamani yoyote. Kama sehemu kubwa ya vitabu vinavyochapwa ingesomwa, chanzo cha maadili potofu kingezuiwa, chanzo kile kinachofanya kazi ya kutisha ya kuhafifisha akili na kupotosha moyo. Hakuna aliyethibitika katika kanuni sahihi kiasi cha kuwa salama na majaribu. Machapisho haya yasiyo na thamani yanapswa kutupiliwa mbali kwa ujasiri.

> *Akili huwa imeathirika kwa kiasi kikubwa kutokana na yale inayojilisha.*

Hatuna kibali kutoka kwa Bwana cha kujihusisha katika kuchapa au kuuza machapisho hayo [yasiyofaa]; kwa kuwa ni njia ya kuharibu roho za wengi. Ninafahamu ninachokiandika, kwa kuwa jambo hili limekuwa likifunuliwa kwangu. Hebu wale wanaouamini ukweli wa wakati huu wasijihusishe katika kazi hiyo, wakifikiria kujipatia fedha. Bwana ataweka pepo mbaya aharibuye matumaini kwenye njia zinazotumika kupatikana [kwa machapisho hayo]; atayatawanya zaidi kuliko yanavyokusanywa.

Kuna daraja jingine la vitabu, linaloambukiza zaidi kuliko ukoma, la kufisha zaidi kuliko mapigo ya Misri, ambalo nyumba zetu za vitabu zinapaswa kujikinga nalo. Kwa kukubali kazi ya biashara, hebu wawe macho, isije ikawa mambo yanayowasilisha sayansi ile ile ya shetani yakaruhusiwa katika taasisi zetu. Hebu machapisho yaliyo na nadharia zinazoharibu moyo za kupumbaza, umizimu, ukatoliki wa Kirumi au siri zingine za uovu zisipate nafasi katika nyumba zetu za uchapaji.

Hebu waajiriwa wasishike chochote kitakachopanda mbegu moja ya mashaka kuhusiana na mamlaka au usafi wa Maandiko. Hebu dhana za ukafiri zisiwekwe mbele ya

vijana, ambao akili zao zinakamata kwa wepesi jambo lolote jipya. Hata ilipwe kwa kiasi kikubwa sana cha namna gani, kazi kama hiyo itachapwa kwa hasara isiyoelezeka.

Kuruhusu mambo ya namna hii kufanyika kupitia taasisi zetu ni kuweka mikononi mwa waajiriwa na kuwasilisha kwa ulimwengu tunda la mti wa maarifa uliokatazwa. Ni kumwalika Shetani aje ndani, na sayansi yake inayologa, ni kupenyeza kanuni zake kwenye taasisi zile zile zilizopangwa kuendeleza kazi takatifu ya Mungu. Kuchapa vitu vyenye tabia hii itakuwa sawa na kujaza risasi kwenye bunduki za adui na kuzikabidhi mikononi mwao, ili zitumike dhidi ya ukweli.

Unadhani Yesu atasimamia uanzishwaji wa nyumba za kuchapa na kufanya kazi kupitia akili za wanadamu na malaika wake wamtumikiao; unadhani kwamba atafanya ukweli unaotoka kwenye nyumba zetu za uchapaji kuwa nguvu ya kuonya ulimwengu, ikiwa Shetani anaruhusiwa kuharibu akili za wafanyakazi papo hapo kwenye taasisi? Je baraka za Mungu zaweza kuandamana na machapisho yatokayo kwenye nyumba ya uchapaji wakati kutoka nyumba hizo hizo za uchapaji kunazalishwa mafundisho ya uwongo na madanganyo ya kishetani? Je! Chemchemi katika jicho moja hutoa maji matamu na maji machungu? Yakobo 3:11.

Mameneja wa taasisi zetu wanatakiwa kutambua kwamba katika kupokea nyadhifa zao wanawajibika kwa chakula cha akili kinachotolewa kwa wafanyakazi wakati wakiwa kwenye taasisi. Wanawajibika kwa tabia inayotengenezwa na vitu vinavyotoka kwenye mitambo yetu. Wataitwa kutoa hesabu kwa ajili ya mvuto uliozalishwa na machapisho yaliyotoka kwenye mitambo yetu, kwa ajili ya uchafuzi wa wafanyakazi, au kwa ajili ya kuipotosha dunia.

Ikiwa mambo haya yanaruhusiwa katika taasisi zetu, itakuja kugundulika kwamba haitakuwa rahisi kuizima nguvu isiyoelezeka ya dhana ya kishetani. Kama mjaribu ataruhusiwa kupanda mbegu zake za uovu, zitaota na kuzaa matunda. Patakuwepo mavuno yake katika taasisi zile zile ambazo zilianzishwa na fedha za watu wa Mungu ili kuendelesha kazi yake. Itasababisha kutuma ulimwenguni kundi la wasomi makafiri, badala ya watendakazi wa Kikristo.


Katika mambo haya uwajibikaji haupo kwa mameneja tu bali na kwa waajiriwa pia. Ninalo neno la kusema kwa kila mfanyakazi wa kila nyumba ya uchapaji iliyoanzishwa katikati yetu: Kwa kadri unavyompenda na kumcha Mungu, kataa kuwa na chochote kinachohusiana na maarifa ambayo Mungu alimuonya Adamu asiwe nayo. Hebu wale wanaopanga mitambo wakatae kuseti sentensi ya mambo hayo. Hebu wahariri wakatae kusoma, wachapaji wakatae kuchapa, na wafungaji mitambo wakatae kufunga. Ukiombwa kushughulikia mambo kama hayo hebu ita mkutano wa wafanyakazi kwenye taasisi, ili wawe na uelewa kwa nini mambo kama hayo yanafanyika. Wale walio na madaraka katika taasisi hizo wanaweza kudai kuwa hustahili [kufanya hayo] na kwamba mameneja watayapanga mambo hayo. Lakini unastahili na unawajibika kutumia macho yako, mikono yako, na akili zako. Vitu hivi viliwekwa na Mungu kwako ili uvitumie kwa ajili yake, siyo kwa huduma ya Shetani.

Wakati vitu vyenye makosa vinavyopingana na kazi ya Mungu vinapochapwa kwenye nyumba zetu za uchapaji, Mungu anawawajibisha siyo wale tu wanaoruhusu Shetani kuweka mtego wa kunasia roho, bali wale wote ambao kwa namna moja au nyingine walishiriki kazi ya majaribu.

Ndugu zangu mlio katika nyadhifa za uwajibikaji, kuweni macho msije mkawafungia wafanyakazi wenu kwenye gari la ushirikina na mafundisho ya uwongo. Hebu msizifanye taasisi zilizoagizwa na Mungu kupeleka ukweli uletao uhai kuwa mawakala wa kusambaza makosa yaharibuyo roho.

Hebu nyumba zetu za uchapaji, kuanzia kwa zile ndogo hadi zile kubwa, zikatae kuchapa hata mstari mmoja wa mambo hayo yanayotiliwa shaka. Hebu na ieleweke kwa wote tunaofanya nao kazi kwamba kutoka kwenye taasisi zetu zote za uchapaji machapisho yoyote yenye sayansi ya Shetani hayapewi nafasi.

Tumeletwa kuungana na ulimwengu si ili tuchachuliwe na uongo wa kidunia, bali kwamba, kama mawakala wa Mungu tuweze kuuchachua ulimwengu kwa ukweli.





# Makala ya Watoto

## *Mambo ya Mungu*

R. Mercy Chebichiy

Kulikuwa na mfalme aliyeitwa Belshaza. Alikuwa mwana wa mfalme Nebukadneza, na baadaye akawa mfalme wa Babeli. Siku moja mfalme Belshaza aliamua kuandaa karamu ya watumishi wake maelfu. Kwenye karamu hii, watu "walikunywa divai, wakaisifu miungu ya dhahabu, na ya fedha, na ya shaba, na ya chuma, na ya mti, na ya mawe." Wakati karamu ikiendelea, aliamuru vyombo vya dhahabu na shaba, ambavyo baba yake mfalme Nebukadneza alikuwa amevichukua kutoka hekalu la Yerusalemu, viletwe ili viweze kutumiwa kwenye karamu hii. Jambo hili halikumpendeza Bwana, na wakati karamu ikiwa inaendelea, vidole vya kiganja cha binadamu vikatokea na kuandika ukutani; MENE, MENE, TEKELI, NA PERESI, ambayo tafsiri yake ni kuwa; Mungu ameuhesabu ufalme wako na kuukomesha. Umepimwa katika mizani nawe umeonekana kuwa umepunguka. Ufalme wako umegawanyika, nao wamepewa Wamedi na Waajemi. Usiku ule ule, mfalme Belshaza aliuawa na ufalme wake ukachukuliwa na Dario Mmedi. Kisa hiki kutoka Danieli 5 kinatupatia mfano wa kile kinachotokea wakati mambo matakatifu yanapotumiwa kwa makusudi yasiyo matakatifu.

Kuna tukio lingine lililotokea, mwanzoni mwa karne ya ishirini, wakati watu wa Mungu walipotumia mambo fulani matakatifu kwa makusudi yasiyo matakatifu. Desemba 30, 1902, kule Battle Creek, jambo fulani lisilo la kawaida lilitokea. Nyumba ya kuchapa vitabu ya Review and Herald, iliungua moto. Hii ilitokea jioni, wakati watu walipokuwa wanafunga kazi. Mlinzi wa usiku alikuwa amekagua jengo na kila kitu kilikuwa sawa, lakini hatimaye jengo lilishika moto! Mitambo na vitabu vilivyokuwa mitamboni vyote viliungua moto. Zimamoto walikuja na kujaribu kuzima moto lakini hawakufanikiwa. Mkuu wa kitengo cha Zimamoto aliyekuwa anaongoza timu ya wazima moto alisema, "Kuna jambo fulani lisilo la kawaida kuhusu mioto yenu ya ki SDA, kila maji yanapopulizwa yanakuwa kama mafuta ya taa." — Barua ya B. P. Fairchild kwa A. L. White, Disemba 4, 1965.

Kabla ya moto, Ellen White, mtumishi wa Mungu, alikuwa ameandika mara kadhaa jumbe za kuwaonya viongozi wa nyumba ya uchapaji. Badala ya wao kusikiliza maonyo, [walipuuza na] hali ya mambo ikaendelea kuwa mbaya. Walikuwa wameanza kuchapa kazi ambazo zisingeleta utukufu kwa Mungu; kama vitabu vinavyokosoa dini, vitabu kuhusu uchawi n.k. Watu waliokuwa wanafanya pale pia hawakuwa wanawakilisha tabia ya Kristo. Moto ulisababisha hasara kubwa, ambapo mitambo ya thamani, vitabu vilivyokuwa tayari vimeshachapwa, vyote viliangamizwa na moto.

Ellen White katika barua aliyomwandikia mtoto wake wa kiume, anaandika; "Oh najisikia vibaya sana, kwa sababu . . . Bwana ameruhusu hili, kwa sababu watu wake hawakusikia maonyo yake, na kutubu, na kuongoka . . ." Lt 214, 1902.

Tunapochukua mambo matakatifu na kuyatumia kwa makusudi yasiyo matakatifu, Mungu hafurahishwi. Unaweza kupiga picha nini kingetokea kama maonyo yangesikilizwa? Biblia hutuambia, "ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao." 2 Mambo ya Nyakati 7:14

(Kisa cha Belshaza kinapatikana katika Sura ya 5 ya Danieli, hadithi hiyo nyingine inaweza kusomwa kwa kina kutoka kwa Makala ya Arthur L. White, yenye kichwa cha "The Story of the Review and Herald Fire," inayopatikana kwenye Review ya Disemba 8, 1977.)

KNOWLEDGE · TRUTH · SERVICE

ADVENTIST UNIVERSITY OF AFRICA

DEVELOPING LEADERS

SPECIAL OFFER

# SCHOOL OF POSTGRADUATE STUDIES

INTRODUCING

### A. A Special Promotional Offer For:

- Master of Science in Applied Computer Science
- Master of Business Administration
- Master of Public Health

### B. Schedule and duration of the programme

- Evening/Sunday/Regular Cohort Classes
- The duration of the programme is two years.

### C. Admission Requirements:

AUA is open to all qualified applicants irrespective of color, race, ethnic identity, religion, gender or national origin. The following Admissions requirements applies. Applicants must hold a bachelor's degree with a minimum CGPA of 2.50 & above on a 4-point scale (Second class lower).

### D. Tuition Fee:

This is a special offer and the tuition fee for this offer will be 60 USD per credit instead of the regular 117 USD per credit. The program begins January 27, 2020 subject to making the class size. Application deadline is December 6, 2019.

### E. Place of instruction:

The place of instruction is the main campus of the Adventist University of Africa at Ongata Rongai. This is a serene environment for academic work. All facilities needed for academic work such as ultra-modern library, fast internet, classrooms with comfortable seating are all available.

### F. Download application form from:

https://www.aua.ac.ke/index.php/2013-06-12-05-25-06/2013-06-12-06-30-31/downloadable-application-forms.html fill, scan and submit to **admissions@aua.ac.ke**

### G. For inquiries contact:

a. **The Dean,** spsdean@aua.ac.ke
b. **Registrar,** registrar@aua.ac.ke
c. **Admission,** admissions@aua.ac.ke
d. **Telephone:** +254-736 656 843 (WhatsApp)
e. **For on campus accommodation contact +254-786500750**

| Fees in KES (USD) | YEAR 1 | | YEAR 2 | |
|---|---|---|---|---|
| | First Semester | Second Semester | Third Semester | Fourth Semester |
| | 15 CR | 15 CR | 15 CR | 6 CR |
| Tuition @ 6,000 ($60) per credit | 90,000 ($900) | 90,000 ($900) | 90,000 ($900) | 36,000 ($360) |
| Registration Fee | 7,500 ($75) | 7,500 ($75) | 7,500 ($75) | 7,500 ($75) |
| Library Fee | 10,000 ($100) | 10,000 ($100) | 10,000 ($100) | 10,000 ($100) |
| ICT Fee | 10,000 ($100) | 10,000 ($100) | 10,000 ($100) | 10,000 ($100) |
| Examination Fee | 2,000 ($20) | 2,000 ($20) | 2,000 ($20) | 2,000 ($20) |
| Research Conference Fee | 5,000 ($50) | 5,000 ($50) | 5,000 ($50) | 5,000 ($50) |
| Total | 124,500 ($1,245) | 124,500 ($1,245) | 124,500 ($1,245) | 70,500 ($705) |
| Sub Total | | | | 444,000 ($4,444) |
| Thesis/Project (Supervision) | | | | 50,000 ($500) |
| Graduation | | | | 40,000 ($400) |
| **TOTAL (All-inclusive fee for the program)** | | | | **534,000 ($5,340)** |

**The date to begin the program is January 27, 2020 subject to making the class size.**




Tutembelee kakika chuo kikuu cha
Adventist University of Africa
Advent Hill, Magadi Road, Ongata Rongai, Kenya

www.aua.ellenwhite.org
www.egwwritings.org

Ellen G. White Estate Branch Office - AUA

@egweboaua

Ili uweze kupata Mambo Muhimu kwa Kiingereza au Swahili, tuma ombi kwa **egwebo@aua.ac.ke** au utupigie simu kwa **+254-733-333-451/2**

**Ofisi za Utafiti za E. G. White Estate Barani Afrika**

**ECD: University of Eastern Africa - Baraton,**
Eldoret, Kenya
egwrc@ueab.ac.ke

**SID: Helderberg College,**
Cape Town, South Africa
clarkec@hbc.ac.za

**WAD: Babcock University,**
Ilishan Remo, Ogun State, Nigeria
egwsdarc@babcock.edu.ng